# GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

*(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)*

**Sehemu ya CXXII Nam. 6487** **16 Septemba, 2013** **Bei Shs. 3,000/=**

*Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti* *Hutolewa kila Ijumaa*

**YALIYOMO** *Ukurasa*

Mswada wa Sheria ya kuanzisha Baraza la
Vijana la Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo............... 341

**SEHEMU YA SHERIA**

Tangazo la Mswada uliyotajwa hapo chini umetangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili

**Tangazo la Mswada**

Nam. :- Mswada wa Sheria ya kuanzisha Baraza la Vijana la Zanzibar.

---

**T A N G A Z O**

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanza tarehe 9 Oktoba, 2013 kwa kusomwa kwa mara ya kwanza na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

**ZANZIBAR** (Dkt. ABDULHAMID Y. MZEE)
16 Septemba, 2013 ***Katibu wa Baraza la Mapinduzi na***
***Katibu Mkuu Kiongozi***.

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga Chapa, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

**MSWADA**
***wa***

**SHERIA YA KUANZISHA BARAZA LA VIJANA LA ZANZIBAR**

**UMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

**SEHEMU YA KWANZA**

**UTANGULIZI**

Jina fupi na tarehe ya kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajuilikana kama Sheria ya Kuanzisha Baraza la Vijana la Zanzibar na itaanza kutumika tarehe ambayo itatangazwa na Waziri katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Ufafanuzi

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Baraza" maana yake ni Baraza la Vijana la Zanzibar kuanzia ngazi ya Kitaifa hadi ngazi ya Shehia lililoanzishwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria hii;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Vijana katika Wizara yenye dhamana kushughulikia masuala ya Vijana;

"Waziri" maana yake ni Waziri anaehusika na masuala ya Vijana;

"Katibu Mkuu" maana yake ni Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana kushughulikia masuala ya Vijana;

"Wizara" maana yake ni Wizara yenye dhamana kushughulikia masuala ya Vijana;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Kijana" maana yake ni mtu mwenye umri baina ya miaka 15 na 35;

"Wanachama" maana yake ni wanachama waliotajwa katika kifungu cha 4 cha sheria hii;

"Mualikwa kiofisi"maana yake ni wageni waalikwa ambao watatokea katika Taasisi za Serikali kuhudhuria Mkutano wa Baraza;

"Kiongozi Mtendaji wa chama cha Siasa" maana yake ni ni mtu mwenye nafasi ya uongozi wa ngazi yoyote katika chama cha kisiasa;

"Mzanzibari" ina maana sawa na ilivyoelezwa katika Sheria ya Mzanzibari Nam. 5 ya 1985.

## SEHEMU YA PILI
## BARAZA LA VIJANA LA ZANZIBAR

Kuanzishwa kwa Baraza la Vijana.

**3.**(1) Kunaanzishwa Baraza la Vijana kwa kifupi "ZYC" ambalo litakuwa ni chombo kinachojitegemea na litakuwa:

(a) lina hadhi ya kisheria na uwezo wa kurithiwa na muhuri wake rasmi;

(b) na uwezo wa kushitaki na kushitakiwa;

(c) na uwezo wa kumiliki na kununua, kupata na kuuza mali inayohamishika na isiyohamishika na linaweza kupokea zawadi,gawio,na msaada kwa jina lake.

(2) Baraza litakuwa katika mpangilio wa muundo ufuatao:

(a) Baraza la Vijana Taifa,

(b) Baraza la Vijana Wilaya, na

(c) Baraza la Vijana Shehia

Uwanachama kwa Baraza.

**4.**(1) Uwanachama kwa Baraza utakuwa wazi kwa vijana wote kupitia Mabaraza yao yaVijana Shehia.

(2) Kijana yeyote anaeyakubali malengo ya Baraza anaweza kuomba uwanachama kwa kujaza fomu ya maombi ambayo itatolewa na Mabaraza ya Vijana Shehia.

(3) Mwanachama wa Baraza atakuwa na haki na wajibu ifuatavyo:

(a) Kuchagua na kuchaguliwa;

(b) Kutoa maoni, mapendekezo na ushauri kwa Baraza;

(c) Kuhudhuria vikao kwa wakati na mahali uliopangwa;

(d) Kuwa muamimifu na mkweli;

(e) Kutunza siri za taarifa zote za siri za Baraza;

(f) kuwa ni mfano kwa wengine kiutekelezajii katika kuhamasisha masuala ya vijana, Sheria, Sera na mipango; na

(g) kulipia ada za uwanachama na malipo mengineyo.

(4) Mwanachama au kiongozi wa Baraza anaweza kusimamishwa au kuondoshwa katika uongozi au uwanachama na Kamati ya Nidhamu kutokana na sababu zifuatazo:

(a) kwa uvunjifu mkubwa wa masharti,mwenendo na Kanuni za Baraza;

(b) kutiwa hatiani kwa kosa la udanganyifu, kughushi,kusambaza nyaraka za kughushi,au kufanya kosa lolote katika makosa yanayohusiana na rushwa na masuala ya kiuchumi

(5) Mwanachama au kiongozi atasita kuwa mwanachama kutokana na yoyote katika sababu zifuatazo:

(a) kifo;

(b) kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kiofisi kutokana na kukosa uwezo kimwili au kiakili kulikothibitishwa na Daktari wa Serikali mwenye mamlaka;

(c) kiongozi mtendaji katika chama cha Siasa;

(d) kuwa na tabia mbaya au mwenendo mbaya;

(e) ametiwa hatiani kwa makosa ya rushwa au ya kimaadili;

(f) kwa kufikia umri wa miaka 35 na zaidi;

(g) kwa kutoa notisi ya siku thalathini ya kujiuzulu kwa Katibu.

## SEHEMU YA TATU
## MALENGO NA UWEZO WA BARAZA

Malengo ya Baraza.

**5.** Baraza linalazimika kuwa na malengo yafuatayo:

(a) kuwajenga vijana kuutambua utaifa wao, hali ya umoja na mshikamano na pia kujiheshimu na pia kuifaham kwa kina jamii, kiuchumi, hali halisi kiutamaduni na upeo wake;

(b) kufanya kazi kama ni jukwaa na kiungo wakilishi kwa masuala ya vijana katika Zanzibar;

(c) kushajiisha kujengewa uwezo vijana ili kuwafanya wazalishaji katika jamii;

(d) kuwakilisha maslahi ya vijana ndani na nje ya nchi.

Kazi za Baraza.

**6.** Baraza litakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kushauri na kushauriana na Wizara katika masuala yote ya vijana na mipango ya maendeleo;

(b) kushajiisha upatikanaji wa haki za vijana kupanua wigo endelevu wa maendeleo ikijumuisha sera ,kanuni, sheria, mambo ya kimisingi na mipango;

(c) kuwezesha na kuimarisha mashirikiano miongoni mwa jumuiya zilizosajiliwa za vijana kitaifa ,kikanda na kimataifa;

(d) kuandaa,kusimamia na kutathmini mipango iliyoanzishwa na vijana ambayo yanaweza kupimwa baadae na jumuiya za vijana sambamba na mipango ya Taifa;

(e) kusaidia na kushajiisha vikundi vyenye maslahi na maendeleo ya vijana katika kuazisha mafunzo kwa vijana na mipango ya maendeleo na utafiti ili kuunga mkono mipango iliyoshuhudiwa ya vijana na kukuza utumiaji wake;

(f) kwa kushirikiana na Wizara kuandaa nyaraka mbalimbali na kueneza taaluma iliyopatikana na mifano ya matendo ya kuigwa yanayohusiana na mipango ya vijana;

(g) kuhamasisha na kusambaza raslimali katika kuunga mkono utekelezaji wa mipango ya vijana na kuimarishia uwezo vikundi au jumuiya za vijana;

(h) kuanzisha, kuendesha na kusimamia miradi yenye na isiyo letea faida katika kuunga mkono maendeleo ya Vijana kama itakavyoonekanwa inafaa;

(i) kupanga na kuendesha mikutano ya Baraza la vijana; na

(j) Kufanya kazi nyenginezo kama ambavyo Baraza litaona inafaa kufuatana na malengo yake.

Uwezo wa baraza.

**7.** Katika kuhakikisha kuwa linafanya kazi zake kiufanisi kwa mujibu wa Sheria hii, Baraza litakuwa na uwezo wa:

(a) kuajiri watendaji wa Baraza kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma au Sheria nyengine yoyote inayohusiana na hayo katika Zanzibar,

(b) kuanzisha vitega uchumi au kuzishughulikia fedha ambazo bado hazijahitajika kimatumizi kwa dhamana na katika njia nyengine itakayoona inafaa na kubadilisha au kufanikisha vitega uchumi hivyo;

(c) kusimamia, kuhakikishia usalama, kukodisha, kuondosha, kuweka rehani,au kwa njia nyengine kuzifanyia kazi mali za Baraza kwa mujibu wa sheria zilizopo na taratibu za nchi;

(d) kupokea michango au hiba iwe ni fedha au mali nyengine kutoka kwa mtu au taasisi kwa ajili ya kuendeleza utekelezaji wa malengo yake,isipokuwa pale ambapo mtu au taasisi hiyo wanajihusisha na matendo yaliyo kinyume na sheria au yaliyo kinyume na maadili;

(e) kutangaza kila baada ya muda umahiri au maelezo mengine ambayo yataonekana ni muhimu kwa ajili ya kuyatukuza malengo ya Baraza; na

(f) kuthibitisha na kuidhinisha mipango ya vijana.

Uwezo wa waziri.

**8.** Waziri anaweza kutoa maelekezo na ushauri kwa Baraza kuhusiana na utekelezaji wa kazi itakapotokea umuhimu wa kufanya hivyo kwa maslahi ya Vijana.

## SEHEMU YA NNE
## MUUNDO NA VYOMBO VINAVYOUNDA BARAZA

Baraza la vijana Taifa.

**9.** Kutakuwa na Baraza la Vijana Taifa ambalo litakuwa vyombo vifuatavyo:

(a) Mkutano Mkuu Taifa;

(b) Baraza la Watendaji;

(c) Sekretariet.

Mkutano Mkuu Taifa.

**10.**(1) Mkutano Mkuu Taifa ni chombo cha ngazi ya juu cha kufanya maamuzi katika Baraza la Vijana la Zanzibar.

(2) Mkutano Mkuu Taifa utakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti wa Baraza Mkoa,Katibu na wanachama watatu kutoka kila mkoa wa Zanzibar kwa kuzingatia jinsia;

(b) Wanachama wote wa Baraza la Watendaji;

(c) wakilishi wawili wa vijana waliochaguliwa kutoka mtandao wa umoja wa wanafunzi wa Zanzibar;

(d) Wawakilishi wawili vijana waliochaguliwa kutoka mtandao wa jumuiya za vijana; na

(e) vijana wawili wanowawakilisha vijana wenye ulemavu walioteuliwa na Waziri.

(3) Mkutano Mkuu Taifa utakuwa na wanachama wafuatao waalikwa ambo hawatakuwa na haki ya kupiga kura:

(a) Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana kushughulikia masuala ya vijana Zanzibar;

(b) Mkurugenzi wa Idara inayohusika na masuala ya vijana Zanzibar;

(c) Watendaji wawili wa Serikali ambao wataalikwa kutokana na utaalamu wao ili kuunga mkono Mkutano Mkuu Taifa.

(4) Mkutano Mkuu Taifa utakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kuthibitisha mipango ya Baraza;

(b) kupokea,kutathmini na kuthibitisha taarifa za Baraza;

(c) kumchagua Mwenyekiti na Makamo Mwenyekiti;

(d) kuwachagua wanachama saba wa Baraza la Watendaji la Baraza kwa kuzingatia kwamba angalau wanachama watatu kati ya wanachama saba wawe ni wanawake.

(5) Mkutano Mkuu Taifa utafanya mkutano wake mara moja katika kila mwaka na mkutano huo utahudhuriwa na wanachama wote wa Mkutano Mkuu.

(6) Mkutano Mkuu Taifa unaweza kufanyika wakati wowote pindi ikihitajika kufanya hivyo.

Baraza la Watendaji.

**11.**(1) Baraza litakuwa na Baraza la Watendaji ambalo wanachama wake watachaguliwa na Mkutano Mkuu Taifa na litakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti;

(b) Makamo Mwenyekiti;

(c) wanachama saba waliochaguliwa na Mkutano Mkuu Taifa; na

(d) Katibu Mtendaji.

(2) Baraza la Watendaji litafanya kazi zifuatazo:

(a) kusimamia na kuratibu kazi za kila siku za Baraza;

(b) kutekeleza maazimio yaliyowekwa na Mkutano Mkuu Taifa;

(c) kupokea,kufanya mapitio, na kthibitisha mipango ya muda, Bajeti na taarifa;

(d) kufatilia na kutathmini utelelezaji wa mipango;

(e) kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekezaji kwa Mkutano Mkuu Taifa; na

(f) kuandaa kuratibu na kuthibitisha chaguzi za uongozi wa Baraza.

(3) Baraza la Watendaji litafanya mkutano katika kila robo ya mwaka isipokuwa kutakapokuwa na kikao cha dharura, ambacho kinaweza kufanyika wakati wowote kutakapohitajika kufanya hivyo .

(4) Mkutano utahudhuriwa na wanachama wote wa Baraza la Watendaji

Sekretariet ya Baraza.

**12.**(1) Kutakuwa na Sekretariet ya Baraza ambayo itaongozwa na Katibu Mtendaji ambae atateuliwa na Rais

(2) Katibu Mtendaji atakuwa Mtendaji Mkuu wa Baraza.

(3) Sekretariet itajumuisha wakuu wote wa Idara za Baraza la vijana Taifa na itafanya kazi zifuatao:

(a) kuandaa ajenda za Mkutano Mkuu Taifa na Baraza la Watendaji kwa kushauriana na Mwenyekiti;

(b) kuandaa na kuwasilisha taarifa za mipango ya utekelezaji kwa kila kipindi, bajeti, na mipango kazi kwa Baraza la Watendaji;

(c) kuchukua kumbukumbu za mikutano;

(d) kuhifadhi nyaraka na kumbukumbu za Baraza;

(e) kumsaidia mwenyekiti kusambaza taarifa za mikutano;

(f) kutekeleza maelekezo yote yaliyotolewa na Baraza la Watendaji kwa mujibu wa Sheria hii;

(g) kuajiri wafanyakazi kwa niaba ya Baraza; na

(h) kutekeleza kazi za kila siku za Baraza.

(4) Kwa mujibu wa sheria hii Baraza linaweza kuiwekea Secratariet utaratibu wa utendaji kazi wake.

Baraza la Vijana Wilaya.

**13.** Kunaanzishwa Baraza la Vijana Wilaya katka kila wilaya ambalo litakuwa na muundo ufuatao:

(a) Mkutano Mkuu Wilaya, na

(b) Kamati Tendaji Wilaya.

Mkutano Mkuu Wilaya.

**14.**(1) Mkutano Mkuu Wilaya utakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti na Makamo Mwenyekiti;

(b) Wanachama wote wa Kamati Tendaji Wilaya;

(c) Afisa wa Vijana Wilaya kwa nafasi yake kiofisi ambae atakuwa ni sekretari wa Baraza la Vijana Wilaya; na

(d) Wenyeviti kutoka kila Baraza laVijana Shehia

(2) Mkutano Mkuu Wilaya utafanya kazi zifuatazo:

(a) kuthibitisha Mipango ya Baraza;

(b) kupokea, kutathmini na kuthibitisha taarifa za vipindi za baraza;

(c) kuchagua mwenyekiti na Makamo Mwenyekiti wa Baraza laVijana Wilaya; na

(d) kuwachagua wanachama saba wa Kamati Tendaji Wilaya kwa kuzingatia kwamba angalau watatu kati ya wanachama saba hao wawe wanawake na mmoja kutoka Vijana wenye ulemavu.

(3) Mkutano Mkuu Wilaya utafanya vikao vyake mara moja kwa mwaka na utahudhuriwa na wanachama wa Mkutano Mkuu Wilaya.

(4) Mkutano Mkuu Wilaya unaweza kufanya kikao wakati wowote kukiwa kunahitajika kufanywa hivyo.

**15.**(1) Kutakuwa na Kamati Tendaji Wilaya katika kila Wilaya ya Zanzibar na itakuwa na wajumbe wafuatao: Kamati Tendaji Wilaya.

(a) Mwenyekiti;

(b) Makamo Mwenyekiti;

(c) wanachama saba waliochaguliwa na Mkutano Mkuu Wilaya; na

(d) katibu Baraza la Vijana Wilaya

(2) Kamati Tendaji Wilaya itafanya kazi zifuatazo:

(a) kusimamia na kuratibu kazi za kila siku za Baraza la Vijana Wilaya;

(b) kutekeleza maazimio yaliyowekwa na Mkutano Mkuu Wilaya;

(c) kuandaa, kufanya mapitio, na kuthibitisha mipango ya muda, Bajeti na taarifa;

(d) kufatilia na kutathmini utelelezaji wa mipango katika ngazi ya Wilaya;

(e) kuandaa na kuwasilisha bajeti ya miaka mitatu, taarifa za mipango na utekezaji kwa Mkutano Mkuu Wilaya; na

(f) kuandaa na kuratibu chaguzi za uongozi wa Baraza la Vijana Wilaya.

(3) Kamati Tendaji Wilaya itafanya mkutano katika kila robo ya mwaka isipokuwa pale ambapo pakitokezea dharura ambayo itapelekea waitishe mkutano muda wowote ikihitajika kufanya hivyo.

(4) Mkutano huo utahuduriwa na wanachama wa Kamati Tendaji.

**16.**(1) Kunaanzishwa Baraza la Vijana Shehia katika kila Shehia ambalo litakuwa na jukumu la kusimamia shughuli za kila siku la Baraza. Baraza la Vijana Shehia.

(2) Baraza la Vijana Shehia lina muundo ufuatao:

(a) Mkutano Mkuu Shehia; na

(b) Kamati Tendaji Shehia.

Mkutano Mkuu Shehia.

**17.**(1) Mkutano Mkuu Shehia utajumuisha wanachama wote wa Baraza wanaoishi katika Shehia.

(2) Baraza la Vijana Shehia litakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kuthibitisha Mipango ya Baraza;

(b) kupokea, kutathmini na kthibitisha taarifa za vipindi za Baraza;

(c) kuchagua mwenyekiti na Makamo Mwenyekiti wa Baraza laVijana Shehia; na

(d) kuwachagua wanachama tisa wa Kamati Tendaji Shehia kwa kuzingatia kwamba angalau watatu kati ya wanachama saba wawe wanawake na mmoja awe kijana kutoka Vijana wenye ulemavu.

(3) Mkutano Mkuu Shehia Wilaya itafanya mkutano kila mwaka isipokuwa pale ambapo pakitokezea dharura ambayo itapelekea wakutane muda wowote ikihitajika ufanya hivyo

(4) Mkutano huo utahuduriwa na wanachama wote wa baraza wanaoishi katika Shehia hiyo.

Kamati Tendaji Shehia.

**18.**(1) Kamati Tendaji Shehia itakuwa na jukumu la kuratibu na kusimamia kazi za kila siku za Baraza katika Shehia.

(2) Kamati Tendaji Shehia itajumuisha wajumbe kumi na mbili kama ifuatavyo:

(a) Mwenyekiti na Makamo Mwenyekiti;

(b) Wanachama tisa wa Kamati Tendaji; na

(c) Katibu.

(3) Kamati tendaji Shehia litakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kusimamia na kuratibu kazi za kila siku za Baraza la Vijana Shehia;

(b) kutekeleza maazimio yaliyowekwa na Mkutano Mkuu Shehia;

(c) kuandaa, kufanya mapitio, na kuthibitisha mipango ya muda, Bajeti na taarifa;

(d) kufuatilia na kutathmini utelelezaji wa mipango katika ngazi ya Shehia;

(e) kuandaa na kuwasilisha bajeti ya miaka mitatu, taarifa za mipango na utekezaji kwa Mkutano Mkuu Shehia; na

(f) kuandaa na kuratibu chaguzi za uongozi wa Baraza la Vijana Shehia.

(3) Kamati Tendaji Shehia itafanya mkutano katika kila robo ya mwaka isipokuwa pale ambapo pakitokezea dharura ambayo itapelekea waitishe mkutano muda wowote ikihitajika kufanya hivyo.

(4) Mkutano huo utahuduriwa na wanachama wote wa Kamati Tendaji Shehia.

**SEHEMU YA TANO**
**VIFUNGU VINAVYOHUSIANA NA FEDHA**

Fedha za Baraza.

**19.**(1) Fedha na rasilimali za Baraza zitajumuisha:-

(a) fedha zitakazo idhinishwa na Baraza la Wawakilishi;

(b) ruzuku, zawadi na misaada;

(c) ada za wanachama au fedha zitokanazo na huduma zitolewazo na Baraza;

(d) fedha zinazoweza kwa namna yoyote kulipwa au kuwekezwa kwa Baraza kwa kufuata masharti ya vifungu vya Sheria hii au zinazohusiana au zinazotokana na utekelezaji wa kazi zake.

(2) Fedha na rasililmali za Baraza zitatumika kwa madhumuni ambayo Baraza limeanzishwa na kwa mujibu wa maelekezo ya Baraza.

(3) Baraza litafungua na kuidhibiti akaunti katika Benki itakayoamuliwa na Baraza, na akaunti hiyo itadhibitiwa kwa namna itakavyoamuliwa na Baraza.

(4) Baraza la Vijana la Taifa la Zanzibar litashughulikia na kusimamia masuala yote ya fedha ya Baraza katika ngazi zote

(5) Baraza litatunza kumbukumbu na kwa usahihi hesabu za fedha zote zilizopokelewa na kutumiwa na Baraza kwa ngazi zote.

Mwaka wa fedha.

**20.** Mwaka wa fedha wa Baraza utakuwa miezi kumi na mbili unaoanzia tarehe mosi ya Mwezi Julai na kumalizikia tarehe thelethini ya Mwezi Juni ya kila Mwaka.

Makadirio.

**21.**(1) Baraza ndani ya kipindi cha siku 21 kabla kumalizika kwa mwaka wa fedha litaandaa na kuwasilisha kwa Waziri kwa ajili ya kuthibitisha makadirio ya mapato na matumizi kwa kipindi kinachofuata cha Mwaka wa fedha.

(2) Hakuna matumizi yatakayofanywa kutoka katika fedha za Baraza isipokuwa yawe yameidhinishwa na Katibu Mtendaji

Hesabu na ukaguzi.

**22.**(1) Baraza litahakikisha linaweka na kuhifadhi vitabu sahihi vya hesabu na kundaa ripoti ya maelezo yanayohusiana na shughuli za kifedha kwa mwaka unaofuata wa fedha si zaidi ya miezi mitatu ya mwaka mpya wa fedha.

(2) Hesabu za Baraza zitakaguliwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, au Mkaguzi aliyethibitishwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu, ndani ya siku ishirini na baada ya kwisha kwa mwaka wa fedha.

Ada ya uanachama.

**23.**(1) Kutakuwa na ada ya uanachama na malipo mengine kwa wanachama wote wa Baraza na yatalipwa kwa kupitia Katibu wa Baraza Shehia

(2) Fedha zitazokusanywa kutokana na malipo ya ada ya uanachama zitatunzwa katika akaunti maalum kama itakavyoelekezwa na Baraza na Baraza la Shehia linaweza kuchukua kiasi kwa ajili ya kuendesha shughuli zake ikijumuisha utekelezaji wa mipango ya vijana.

Kuwekeza Mfuko.

**24.** Baraza linaweza kuwekeza fedha zake katika dhamana ambapo Baraza linaweza kuwekeza Kisheria uwekezaji mfuko wa dhamana,au katika dhamana yoyote ambayo Mkutano mkuu Taifa utakuwa na dhamana ya kuidhinisha kila baada ya muda na kuthibitisha.

## SEHEMU YA SITA
## MENGINEYO

Nembo na Muhuri wa Baraza.

**25.**(1) Baraza litakuwa na nembo na muhuri rasmi ambao utakuwa ni alama ya Baraza kwa ngazi zote.

(2) Muhuri wa Baraza utakuwa katika namna itakavyoamuliwa na Kamati Tendaji na utatunzwa na kuhifadhiwa na Baraza.

(3) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti , Katibu Mtendaji wa Baraza au mtu mwengine atakayepewa idhini na Baraza ndio watakaokuwa na uhalali wa matumizi ya muhuri wa Baraza.

Kanuni.

**26.** Waziri anaweza, kwa kushahuriwa na Baraza na kwa kuhakikisha utekelezaji bora wa masharti ya vifungu vya Sheria hii, bila ya kuathiri masharti ya jumla ya Sheria hii kutunga kanuni kuhusiana na:-

(a) kuweka taratibu za kiutawala za Baraza

(b) taratibu za uchaguzi;

(c) taratibu za uajiri;

(d) taratibu za kifedha;

(e) kuweka taratibu zinazoelezea kitu chochote kinachohitajika au kimeruhusika kuwekewa utaratibu, kilicotolewa maelekezo au kinachohusiana na Baraza.

Muda wa uanachama.

**27.**(1) Mwanachama yeyote isipokuwa wale wanachama kwa mujibu wa nafasi zao kiofisi, kwa mujibu wa masharti ya vifungu vya Sheria hii watatumikia ofisi kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu kwa mujibu wa masharti ya uteuzi wao, hata hivyo wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine cha miaka mitatu.

(2) Wajumbe wa Baraza watateuliwa kwa nyakati tofauti ili kuepusha wote kumaliza muda wa kutumikia ofisi kwa wakati mmoja.

Utaratibu wa mkutano.

**28.**(1) Kikawaida Baraza litafanya mikutano yake kwa wakati na sehemu watakayoona inafaa kwa ajili ya kutimiza shughuli zake.

(2) Mwenyekiti, au ikiwa hayupo, Makamo Mwenyekiti anaweza kuitisha mkutano, na ataitisha mkutano maalum wa Baraza kutokana na maombi kwa maandishi kutoka kwa wengi wa wajumbe Baraza.

(3) Mwenyekiti au ikiwa hayupo, Makamu Mwenyekiti ataongoza kila mkutano wa Baraza, na wasipokuwepo wote Mwenyekiti au Makamo Mweneyekiti, wajumbe waliopo watamchagua mjumbe kutoka miongoni mwao kuongoza mkutano.

Uchaguzi na utaratibu za kupiga kura.

**29.**(1) Uchaguzi Mkuu wa Baraza utafanyika katika kila kipindi cha miaka mitatu.

(2) Waziri atatunga kanuni kwa Baraza zinazohusiana na uchaguzi na taratibu za upigaji kura .

Akidi.

**30.** Zaidi ya nusu ya wajumbe wa mkutano watafanya akidi katika mikutano ya Baraza, isipokuwa maamuzi ya mkutano wowote hayatafanywa na wajumbe watakaokuwa chini ya theluthi mbili ya wajumbe waliopo.

Taratibu za nidham.

**31.**(1) Baraza litaunda kamati ya nidhamu, na litaandaa taratibu na kanuni za uchukuaji wa hatua za kinidhamu dhidi ya wanachama wake.

(2) Hakuna atakaechukuliwa hatua za kinidhamu mpaka awe amepewa fursa ya kujieleza kuhusiana na kesi yake na kujitetea mbele ya kamati ya nidhamu.

(3) Kutakuwa na haki ya kukata rufaa dhidi ya maamuzi ya hatua za kinidhamu kwa mkutano mkuu .

Maazimio ya Baraza.

**32.** Maazimio yanayopitishwa katika Mkutano wa Baraza yatahesabiwa kuwa ni halali kwa kuungwa mkono na wingi wa kura za wajumbe waliopo.

Usawa wa kijinsia.

**33.** Baraza litahakikisha usawa wa kijinsia unazingatiwa katika kila mipango na uongozi wa Baraza.

Uongozi wa Baraza.

**34.**(1) Mwenyekiti na Makamo Mwenyekiti wa Baraza ni lazima awe na sifa zifuatazo:-

(a) awe na umri wa angalau miaka kati ya miaka 18 hadi 32;

(b) awe na cheti angalau cha elimu ya sekondari ya kawaida;

(c) awe mwenye tabia nzuri;

(d) awe mzanzibari.

(2) Itakapokuwa Mwenyekiti mwanaume, Makamo Mwenyekiti awe mwanamke na kinyume chake.

(3) Mwenyekiti na Makamo Mwenyekiti watachaguliwa na Mkutano Mkuu na watakuwa ni viongozi na wasimamizi wa kazi za kila siku za Baraza na wataendesha mikutano yote ya baraza katika ngazi husika isipokuwa sekretariet.

(4) Mwenyekiti na Makamo Mwenyekiti watakuwa wasemaji wakuu wa Baraza.

(5) Katibu Mtendaji atateuliwa na Rais na atakuwa mtendaji mkuu na mwenye dhamana ya uendeshaji wa Baraza, na

(6) Katibu Mtendaji atakuwa pia Katibu wa Mkutano Mkuu na wa Kamati Tendaji, na atakuwa na wajibu wa kuitisha na kuwa Mwenyekiti wa mikutano ya sekretariet.

**MADHUMUNI NA SABABU**

Madhumuni ya mswada huu ni kuanzisha Baraza la vijana Zanzibar Baraza ambalo litakuwa ni chombo chenye mamlaka na hadhi ya juu katika kuwakilisha maslahi ya vijana Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kwa mujibu wa Sheria.

Ni muda mrefu umepita ambapo vijana wa Zanzibar wamefanya juhudi za makusudi katika kuhakikisha kuwa wanapata nafasi ya kujiunga pamoja, kusikilizwa na kujieleza kuhusiana na mambo yenye maslahi na wao na Taifa kwa jumla kwa hivi sasa na kwa wakati ujao,

Wizara ya Uwezeshaji,Ustawi waJamii,Vijana Wanawake na Watoto kwa kuamini kwamba ina jukumu la kusimamia na kuratibu Sera, Sheria na miongozo ya Serikali yenye lengo la kujenga mazingira endelevu ya kuwawezesha vijana wa Zanzibar kujiimarisha kiuchumi kiutamaduni na kijamii na kutokana na ukweli kwamba vijana ndio nguvu kazi ya Taifa na kuwa ipo haja na umuhimu wa kuzithamini na kuunga mkono juhudi zao ikiwa ni pamoja na kwenda sambamba na matakwa ya jumuiya za Kimataifa na kikanda yanayotilia mkazo umuhimu wa kuwajengea uwezo vijana ikiwemo kuwa na chombo cha kuwashirikisha katika michakato ya maendeleo katika jamii na uhuru wa kutoa maoni yao, ndipo ilipoona ipo aja ya kukubaliana na vijana kuanzisha chombo hiki ambacho kwa kushirikiana na Serikali kitaweza kuwa na uwakilishi mzuri kwa vijana .

Baraza la vijana linaloundwa kwa mujibu wa Sheria hii litakuwa katika ngazi tafauti ili kupata uwakilishi wa kutosha kuanzia ngazi ya Shehia hadi Taifa.

Nafasi ya uwanachama kwa Baraza itakuwa wazi kwa Vijana wote Wazanzibari waliotimiza sifa kwa mujibu wa Sheria hii wanaoishi katika shehia ambao watakuwa tayari kuyafuata na kuyalinda malengo ya uundwaji wa Baraza.

Mswada huu umegawika katika Sehemu sita na una jumla ya vifungu vifungu 34.

Sehemu ya kwanza inahusu vifungu vya utangulizi na inaelezea jina fupi na kuanza kutumika, na tafsiri za baadhi ya maneno yaliyotumika katika Sheria na izingatiwe kwamba tafsiri ya neno "Baraza" likitajwa ifahamike kama ambavyo imetolewa kwenye tafsiri kuwa inajumuisha Mabaraza katika ngazi zote kuanzia Shehia hadi Taifa.

Sehemu ya Pili ina kifungu nam. 3 na 4.

Sehemu hii inahusiana na mambo mbali mbali ikiwemo uanzishwaji Baraza na imeoneshwa muundo wake halisi wa Baraza kuanzia ngazi ya Shehia hadi ya Taifa, uwanachama kwa Baraza jinsi unavyopatikana na masharti ya upatikanaji wake, haki na wajibu wa mwanachama, vipi mwanachama anaweza kusimamishwa au kundoshwa katika uwanachama au uongozi, na vipi mwachama atasita kuwa mwanachama au kiongozi.

Sehemu ya tatu inahusu Malengo na Uwezo wa Baraza na ina jumla ya vifungu vinne kuanzia kifungu cha 5 hadi 8 ambapo kifungu cha tano kimeeleza malengo hasa ya kuanzishwa Baraza, kifungu cha 6 kimeeleza kazi zitakazofanywa na Baraza, kifungu cha saba kimeeleza uwezo wa Baraza na kifungu cha 8 kimeeleza uwezo wa Mhe. Waziri kwa Baraza ambao ni wa kuweza kuwapa maelezo na ushauri Braza pale itakapoonekana haja ya kufanya hivyo.

Sehemu ya nne inaelezea kuhusu muundo na vyombo vinavyounda Baraza katika ngazi zake tofauti .

Sehemu hii imeazia katika kifungu cha 9 hadi cha 18 pamoja na mambo mengine sehemu hii imeeleza kazi za Baraza katika maeneo hayo, mbali na kazi za jumla za Baraza na vile vile taratibu za kupata watendaji katika Mabaraza hayo na utaratibu wa mikutano.

Sehemu ya tano inahusu masuala ya Fedha na vyanzo vya mapato ya Baraza. Ina vifunngu kuazia cha 19 mpaka 24. Miongoni mwa yaliyoelezwa katika kifungu cha 19 ni vyanzo vya mapato na raslimali za Baraza na katika hali ipi zitatumika, utunzaji wa mahesabu ya Baraza na nani atakuwa na dhamana ya kuushughulikia nakuudhibiti mfuko na raslimali hizo.

Kifungu cha 20 hadi 24 vinaeleza utaratibu wa jumla wa fedha za Taasisi za Serikali ikijumuisha makadirio ya mapato na matumizi utunzaji wa mahesabu, na ukaguzi wa Serikali kufanyika kwa kupitia Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu au Mkaguzi aliyeidhinishwa na Ofisi ya Mdhibiti, matumizi ya mfuko katika kuazisha vitega uchumi ili kuukuza, na chanzo cha mapato yatokanayo na malipo ya uwanachama.

Sehemu ya Sita imejumuisha vifungu vya jumla kuanzia kifungu cha 25 hadi cha 34 vyenye masharti mbalimbali yanayohusiana na Sheria hii ikiwemo Baraza kuweka nembo na muhuri rasmi najinsi gani au vipi muhuri huo utatambulika matumizi yake kisheria, kifungu cha 26 kinaelezea uwezo wa Mhe.Waziri kutunga kanuni, kifungu cha 27 kimeainisha muda wa kutumikia Baraza na utaratibu wa kuweka muda kutumikia Baraza, taratibu za uendeshaji vikao, uchaguzi na taratibu za upigaji kura, kifungu cha 30 akidi, kifungu cha 31 hatua za kinidhamu na kifungu cha 32 vipi yatafikiwa maazimio ya vikao vya Baraza, kifungu cha 33 usawa kijinsia, na kifungu cha 34 uongozi wa Baraza.

**ZANZIBAR**
16 Septemba, 2013

(ZAINAB OMAR MOHAMMED)
***Waziri wa Uwezeshaji,Ustawi wa Jamii,Vijana Wanawake na Watoto Zanzibar***